**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU UWASILISHWAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumbaji wa kila kitu hapa Duniani na huko Akhera, kwa kutujaalia kuwa hai na wazima wa afya ambae taufiki yake ametukutanisha tena katika Baraza hili la Kumi na Moja kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar hususan katika juhudi za kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika** aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuzungumzia machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa Kauli ya Serikali inayohusiana na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025 kama ambavyo Kanuni ya 44 fasili ya (1) aya ya (b) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti, wenye hekima, busara na mipango inayotekelezeka ambayo imekuwa dira katika kusimamia vyema rasilimali za nchi yetu, kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na hatimae kufikia katika maendeleo ya kweli, jambo linalotoa taswira njema kwa wananchi wa Zanzibar kuweza kunufaika na kuimarika kwa maisha ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Juhudi hizo zinadhihirisha wazi kwamba uongozi wake ni "uongozi unaoacha alama".

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa nimshukuru Mzee wetu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalimu Dkt. Haroun Ali Suleiman kwa kuweza kutekeleza matakwa ya

kifungu cha 112 kifungu kidogo cha (5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambacho kwa Mamlaka aliyopewa Mheshimiwa Rais, amemruhusu Mheshimiwa Waziri huyu kuziwasilisha hapa Barazani Ripoti hizi ambazo ndio nyenzo zinazotumiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuchunguza Mapato na Matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Shukrani za dhati ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali, ambao kwa umahiri wao, uzoefu na weledi walionao wameendelea kutoa michango muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa kutambua umuhimu wa michango hiyo, naomba uniruhusu niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | - | Mwenyekiti; |
| 2. Mhe. Mohammed Manzi Haji | - | M/Mwenyekiti; |
| 3. Mhe. Abdulwahab Said Abubakar | - | Mjumbe; |
| 4. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Mjumbe; |
| 5. Mhe. Juma Hassan Thabit (Kaponda) | - | Mjumbe; |
| 6. Mhe Jabu Makame Juma | - | Mjumbe; na |
| 7. Mhe. Simai Mohammed Said | - | Mjumbe; |

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na Wajumbe hao, napenda pia kuishukuru na kuipongeza Sekretarieti ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa kuhakikisha shughuli za Kamati zinafanyika kwa ufanisi na kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo. Uzoefu na ushauri wao wa kitaalamu, kwa kiasi kikubwa umekuwa dira kwa Wajumbe wa Kamati yetu kutekeleza majukumu yao kwa umakini, uweledi na kwa ufanisi mkubwa, hasa ukizingatia Wajumbe wengi wa Kamati hii ni wapya. Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Shaaban Suleiman Juma | - | Katibu; |
| 2. Ndg. Khadija Salmin Awadh | - | Katibu; na |
| 3. Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu. |

Mheshimiwa Spika, Kamati ya PAC inatambua, kuheshimu na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika kuchangia kuimarisha utawala bora ikijumuisha kujenga nidhamu ya ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Rasimali za Umma hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 na Sheria ya Ununuzi wa Umma Zanzibar Namba 2 ya mwaka 2025 zinaelekeza utaratibu na nidhamu ya matumizi yanayohitajika kufanywa na Wizara na Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati yangu ina kila sababu ya kuwapongeza kwa dhati Viongozi na Watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa utekelezaji wa kazi ngumu ya udhibiti na

ukaguzi na hatimae kumudu kuandaa Ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 112 kifungu kidogo cha (5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, amemkabidhi Spika wa Baraza hili, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Ripoti Kumi na Mbili (12) za Ukaguzi ambapo leo hii, rasmi Ripoti hizo zimewasilishwa hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Kamati ya PAC imezipokea Ripoti zote Kumi na Mbili (12), itazifanyia kazi na hatimae kuwasilisha Ripoti yake mbele ya Baraza hili tukufu katika wakati muafaka utakaopangwa kwa ajili hiyo kama inavyoelekezwa na Kanuni zinazotuongoza.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ambazo Kamati yetu imekabidhiwa ni hizi zifuatazo:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Nyumba za Biashara na Makaazi Nyumba 370 za Fidia pamoja na Nyumba za gharama nafuu kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali na Ununuzi wa Vifaa vya Maabara ya ZBS kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025.
5. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani pamoja na Ujenzi wa Kiwanda cha Uchakataji na Usindikaji wa Dagaa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
6. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
7. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari na Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege (AAKIA-TERMINAL 2-2) kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
8. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya na Nyumba za

Wafanyakazi Unguja na Pemba kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
9. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
10. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025;
11. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Majengo ya Biashara, Huduma za Jamii na Maeneo ya Kihistoria kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025; na
12. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Taasisi za Umma kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Hesabu za Serikali inaamini kwamba baada ya kukamilisha mchakato wa kuzifanyia kazi Ripoti hizi, Waheshimiwa Wajumbe watazichangia ipasavyo na hatimae kutoa Maagizo kwa Serikali, na tunaamini kwa usikivu wa Serikali yetu, hatua stahiki zitachukuliwa kwa Watendaji wote watakaohusika na ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia tathmini ndogo ambayo Kamati yetu imeifanya kufuatia uwasilishwaji wa Ripoti hizi, Kamati yetu imebaini mambo ya jumla yafuatayo:-

## 1. KUONGEZEKA KWA IDADI YA RIPOTI ZILIZOWASILISHWA

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya jumla inaonesha wazi kwamba Ripoti zilizowasilishwa mwaka 2024/2025 zimeongezeka kiidadi ukilinganisha na Ripoti ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alizitoa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hii inamaana kwamba katika mwaka wa fedha huu, Mkaguzi ametoa Ripoti zake Kumi na Mbili wakati mwaka wa fedha wa ukaguzi uliopita alitoa Ripoti Kumi na Moja, sawa na tofauti ya Ripoti moja.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwepo utofauti katika idadi ya Ripoti hizi, pia kuna utofauti unaotokana na maudhui yaliyobebwa katika majina ya Ripoti hizo. Hali hiyo imepelekea kuwepo kwa Ripoti Tano ambazo zimelingana kimaudhui. Ripoti zenyewe zinahusiana na:-

1. Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
2. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu;
3. Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Taasisi za Umma;

4. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo; na
5. Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** sanjari na hilo, kuna baadhi ya Ripoti maudhui yake yanatofautiana kulingana na wigo na utekelezaji wa shughuli iliyofanyiwa ukaguzi. Miongoni mwa Ripoti hizo (kwa mwaka jana) zinahusiana na Ukaguzi wa ununuzi wa gari za Serikali, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Miradi ya Wadi, ukaguzi wa kiufundi wa miundombinu ya maji, barabara, ujenzi wa masoko pamoja na ukaguzi wa kiufundi wa ujenzi wa maskuli.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, tathmini ya Kamati imebaini kuwa Ripoti za Ukaguzi wa Kiufundi zimeonekana kuongezeka katika mwaka huu wa ukaguzi 2024/2025. Suala hili, pamoja na mambo mengine, limechangiwa zaidi za uwepo wa kasi kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo Serikali inaitekeleza. Hali hiyo, imepelekea kuwepo kwa Ripoti Sita za Ukaguzi wa Kuifundi katika mwaka huu (2024/2025) ukilinganisha na Ripoti Tano za mwaka jana (2023/2024). Kwa msingi huo, Ripoti zote hizo zinatofautiana kimaudhui isipokuwa Ripoti moja tu ya Ukaguzi wa kiufundi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

## 2. HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huainisha hati alizozitoa kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika Ripoti zake kuu Nne ambazo ni Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea, Ripoti ya Ukaguzi wa Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu pamoja na Ripoti inayohusiana na Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na SMZ na Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea imeainisha uwepo wa jumla ya hati 51 zilitolewa ambapo hati 49 zilikuwa ni hati zinazoridhisha, hati moja ni yenye shaka kwa Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF) na hati moja ni mbaya kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ambapo hata mwaka jana Kampuni hii ilipata hati yenye shaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa hati zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu, kuna jumla ya hati 69 za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo hati 68 zilikuwa ni hati zinazoridhisha na hati moja ilikuwa ni hati yenye shaka kwa Fungu la Hesabu Jumuishi ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Fungu hili

pia limeendelea kupata hati yenye shaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, jumla ya hati 23 zilitolewa ambapo hati 22 ni zenye kuridhisha wakati hati moja ni hati yenye shaka kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Aidha, Mkoa huu hata mwaka jana ulipata hati yenye shaka.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na Ripoti ya Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa, Mkaguzi alitarajiwa kutoa jumla ya hati 47 za ukaguzi. Hata hivyo, amefanikiwa kutoa jumla ya hati 29 zinazoridhisha na kwa bahati mbaya, jumla ya Miradi 18 Mkaguzi hakuweza kuitolea maoni kutokana na kutowasilishwa kwa taarifa za hesabu zao za fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla idadi ya hati zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara na Taasisi za Serikali zimeonesha kuendelea kuongezeka. Hali hii inatokana na Mdhibiti kuzifanyia ukaguzi Wizara, Taasisi na Miradi mingi zaidi ukilinganisha na mwaka jana. Katika mwaka 2024/2025, kuna jumla ya hati 171 zilizotolewa wakati mwaka 2023/2024 kulikuwa na hati za ukaguzi 130 sawa na tofauti ya hati 41. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba kwa kadri matokeo ya ukaguzi yanavyoendelea kutolewa siku hadi siku, Wizara na Taasisi za Serikali zimeendelea kuimarika kiutendaji na kupelekea hati zenye shaka pamoja na hati mbaya kupungua.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo pia imetokana na Watendaji kwa kiasi kikubwa kujaribu kujirekebisha na kasoro ambazo Mkaguzi huziwasilisha kwao. Sambamba na hilo, Taasisi zimekuwa zikitoa ushirikiano kwa Mkaguzi na sio kumfanya adui anapofika katika maeneo yao ya kazi.

## 3. UWASILISHWAJI WA TAARIFA YA HESABU YA MWISHO WA MWAKA (ANNUAL FINANCIAL STATEMENT)

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 119 kifungu kidogo cha (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016, kimezitaka Wizara na Taasisi za Serikali kutayarisha na kuwasilisha Taarifa zao za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Tathmini inaonesha kwamba katika Ripoti za Ukaguzi za mwaka 2024/2025, Wizara na Taasisi nyingi za Serikali zimefanikiwa kuwasilisha Taarifa zao za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ndani ya muda unaotakiwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kuna baadhi ya Taasisi za Serikali zimeshindwa kutekeleza ipasavyo matakwa hayo ya Sheria na kupelekea

kuwasilisha taarifa zao nje ya muda uliowekwa kisheria. Taasisi hizo ni hizi zifuatazo:-

1. Hospitali ya Mnazi Mmoja;
2. Kamisheni ya Utalii;
3. Baraza la Vijana Zanzibar;
4. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara;
5. Kikosi Maalum cha Kuzuia magendo; na
6. Viwanda vya Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia Ripoti yake ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 amebainisha kwamba amefanikiwa kukagua Miradi yote 47 iliyotekelezwa na kugundua kwamba kati ya Miradi hiyo, Miradi 29 iliwasilisha taarifa zao za hesabu kwa mujibu wa masharti ya sheria wakati Miradi 18 ilishindwa kuandaa na kuwasilisha hesabu zao katika Afisi ya Mdhibiti.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo ilipelekea Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo na hatimae kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi wake kwa Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa Miradi ya Maendeleo iliyoshindwa kuwasilisha taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ni pamoja na Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana, Mradi wa Tathmini wa Ubora wa Maji ya Bahari, Programu ya kuendeleza Viwanja, Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji na Programu ya Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji (INDIA).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imesikitishwa na matokeo hayo hasa ukizingatia Miradi hiyo imetekelezwa kwa fedha nyingi na Taasisi zetu zinao Watendaji weledi wanaojua sheria zinataka nini. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango huwa inajitahidi kuwapatia mafunzo Wahasibu wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusiana na mambo tofauti yanayohusiana na uwajibikaji katika kazi zao. Kwa msingi huo, hali hii huonesha kuwepo kwa uzembe na dharau zinazofanywa na watendaji wetu. Hivyo, ni wajibu wa Maafisa Masuul kuhakikisha wanawasimamia vyema watendaji wao ili kasoro kama hizo zisiweze kujitokeza tena.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaeleza kwamba itazipitia Taasisi na Miradi hiyo kwa lengo la kujua uhalisia ulivyo na hatimae kutoa ushauri wake ili ziweze kurekebisha kasoro hizo na kuondokana na hoja za namna hii ambazo hazina sababu za msingi kutokea.

## 4. KUWEPO KWA HOJA ZENYE KUJIRUDIA

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar amebaini dosari lukuki katika Ripoti zake na kuzitolea ushauri ndani yake. Hata hivyo, kiujumla, Kamati yetu imegundua kwamba kuna baadhi ya hoja zimekuwa zikijirudia rudia na kuonekana zimekuwa sugu na hazijafanyiwa kazi ipasavyo. Hali hiyo inaashiria kwamba bado kuna utekelezaji usioridhisha kwa baadhi ya Watendaji wa Serikali na Taasisi zake au kuna ukiukwaji wa taratibu za kisheria zinazohusiana na ununuzi na usimamizi wa fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Hesabu za Serikali inasikitishwa na kushangazwa kwamba pamoja na kubainika dosari kupitia ukaguzi uliopita wa mwaka 2023/2024 na juhudi kadhaa kuchukuliwa ili kasoro hizo ziweze kurekebishwa. Hata hivyo, bado kuna Taasisi zinaonekana hazioneshi mabadiliko ya matokeo chanya kwani dosari ambazo zimeripotiwa katika Ripoti zilizopita, zimeendelea kujitokeza katika Ripoti mpya za mwaka huu. Hali hiyo haitoi taswira nzuri hususan katika utekelezaji wa misingi ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini hayo katika Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu, Ukaguzi wa TEHAMA, Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea na Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia Ripoti hizo, dosari zifuatazo zimebainika kujirudia, miongoni mwa dosari hizo ni:-

1. Kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na miradi;
2. Kukosekana kwa taarifa za ukaguzi wa ndani za mradi;
3. Uwepo wa bakaa ya fedha (za Dola za Kimarekeni au shilingi za Tananzania) ambazo hazijatumika katika mradi au mifuko tofauti;
4. Uwepo wa ongezeko la kazi lililotumia fedha nyingi za Tanzania bila ya kufuata utaratibu;
5. Malipo yaliyolipwa kwa kazi ambazo hazikuwemo katika Mkataba;
6. Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi;
7. Kukosekana kwa idhini ya nyongeza ya mkataba;
8. Kutokuwepo kwa mpango wa mafunzo ya matumizi ya mifumo na usalama wa mitandao kwa wafanyakazi;
9. Kutokushirikishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (Egaz) katika hatua za ujenzi na uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za umma;

10. Kukosekana kwa nyaraka muhimu za ujenzi wa mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi za Umma;
11. Mapato yaliyokusanywa nje ya Mfumo wa ZanMalipo;
12. Kuchelewa kukamilika kwa miradi ndani ya muda uliopangwa;
13. Kuwepo kwa madeni yanayodaiwa na Taasisi za Serikali kwa Taasisi nyengine za Serikali na Taasisi binafsi; na
14. Kutowasilishwa Mikataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia kujirudia kwa hoja za namna hiyo, Kamati ya PAC inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali yanayohusiana na taratibu za ununuzi na usimamizi wa rasimali za umma. Aidha, watendaji waendelee kutoa mashirikiano ya karibu kwa watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanapofika katika maeneo yao ya kazi hususan Maafisa Masuul kwani wao ndio wanaowajibika moja kwa moja na hoja ambazo Mkaguzi anaziibua.

## 5. KUWEPO KWA HOJA ZINAZOHITAJI UTEKELEZAJI WA HARAKA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Hesabu za Serikali imebaini kuwa kuna baadhi ya dosari ambazo Mkaguzi amezibainisha katika Ripoti alizozitoa, kwa namna moja au vyenginevyo, zinahitaji mazingatio ya haraka katika utekelezaji wake. Hii inatokana na ukweli kwamba iwapo Serikali haitokuwa makini au kuchukua hatua za kuzifanyia kazi kwa haraka, zinaweza kusababisha athari katika matokeo yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwamba Serikali yetu ni makini na sikivu. Hivyo itachukua juhudi za makusudi kurekebisha kasoro zilizoibuliwa na Mkaguzi kwa kuzifanyia kazi au kuziondoa na hatimae ufanisi uweze kupatikana. Iwapo hilo litafanyika, changamoto zilizoibuliwa zitaondoka, huduma zilizotegemewa kupatikana zitapatikana, imani ya wananchi wetu kwa Serikali yao itazidi kuimarika, misingi ya utawala bora itatekelezwa ipasavyo na hatimae ukali wa maisha kwa wananchi wetu utapungua kama sio kuondoka kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa dosari au hoja hizo ni: -

1. Kukaribia kikomo cha matumizi ya nyaya za umeme za baharini (sub marine cable);
2. Mfumo wa ZANMUTM kuzalisha control numbers zisizoakisi muda wa kikomo (no standard expiry mechanism);
3. Udhaifu wa udhibiti wa Mfumo wa BAMAS katika kuzuia matumizi yanayozidi Bajeti (Commitment Control);
4. Tofauti katika taarifa za makusanyo ya mapato baina ya Mfumo wa VFMS na ZIDRAS;

5. Mfumo wa VFMS kushindwa kukusanya kodi wa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA);
6. Kutofanya kazi kwa Mfumo wa Kusimamia Taarifa za kuwasili na kuondoka kwa Wageni (GADIS);
7. Ankara za Michango zilizobaki bila ya kulipwa katika Mfumo wa AMMIS bila namba za Udhibiti;
8. Dosari katika muunganiko na udhibiti baina ya Mfumo wa BAMAS na Mfumo wa GERAS;
9. Kukosekana kwa risiti za kielektroniki; na
10. Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndio inayofanya ukaguzi na kujua mambo kadhaa yaliyojitokeza wakati wa kutekeleza kazi zake. Aidha, Afisi hii ndio yenye uelewa wa mbinu tofauti za ukaguzi zinazotumika kitaifa na kimataifa na hatimae kuandaa Ripoti zake ambazo hutofautiana kati ya Ripoti moja na nyengine kulingana na maumbile ya aina ya ukaguzi uliofanywa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati ya Hesabu za Serikali hasa ukizingatia ni Kamati mpya na yenye Wajumbe wapya waliokuwa na fani tofauti. Hivyo, Kamati yetu inaiomba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwapatia Wajumbe wa Kamati hii mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kumudu vyema utekelezaji wa majukumu ya msingi kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 119 fasili ya (3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu kwa heshima na taadhima, inaitaka Serikali kuiingizia kikamilifu fedha za matumizi kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyopanga katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2026/2027 ili nayo iweze kutekeleza lengo hilo la kuwapatia mafunzo Wajumbe wapya wa Kamati ya PAC yatakayoongeza uelewa na umakini wao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiuchunguzi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa naishukuru Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa iliyoipatia Kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake ikiwemo utekelezaji wa kazi hii ya kuchambua na hatimae kutoa maoni au mapendekezo yetu juu ya uwasilishwaji wa Ripoti hizi za Ukaguzi mbele ya Baraza letu. Nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya Maoni ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, naomba kuwasilisha.



**……………………**

Mhe. Kombo Mwinyi Shehe,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC),
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**

********-----********